**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote tunamshukuru Allah (S.W.T) mwingi wa rehma na utukufu, kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la kumi, kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, nakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, kwa jitihada zako na namna unavyoliongoza Baraza hili tukufu kwa ustadi mkubwa. Ni imani yetu kwamba, utaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ufanisi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha Demokrasia katika chombo hiki muhimu.

**Mheshimiwa Spika,**
Pia, naomba kuchukua fursa hii, kumshukuru na kumpongeza kwa dhati Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Naibu Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote kwa jitihada kubwa wanazozichukua katika kulipeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa namna ya pekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kazi kubwa na nzuri wanazozifanya wakati wote wa kazi za Kamati, jambo ambalo limepelekea wepesi kwangu kuweza kuiongoza Kamati hii inayosimamia Wizara muhimu kabisa. Wajumbe wa Kamati wameonesha umahiri, weledi na umakini wa hali ya juu na wameweza kuijadili ipasavyo Bajeti hii na kuhoji mambo mengi ya msingi, kwa lengo la kuhakikisha fedha wanazoidhinisha katika Baraza hili, zinatumika vizuri na kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,**
Napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote waliomo katika Baraza lako Tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi na makundi yaliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wamejenga imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako, na kwa heshima ya kipekee naomba niwatambue Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Mwantatu Mbarak Khamis | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Abdalla Abbasi Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,**
Aidha, Kamati hii inafanyakazi kwa kusaidiwa na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu, msaada wa makatibu hao umekuwa chachu ya mafanikio makubwa ya Kamati hii. Makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 2. | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 3. | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**
Moja kati ya jukumu la msingi la Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimaye kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, sasa kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati, napenda kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo kwa mwaka wa fedha **2022/2023.**

**Mheshimiwa Spika,**
Baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitekeleze jukumu nililopewa na Kamati la kuwasilisha Maoni ya Kamati, mbele ya Baraza lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mwaka huu wa fedha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imepangiwa kutekeleza Programu Kuu Tatu (3) ambapo utekelezaji wake unasimamiwa na Programu Ndogo Tano (5).

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati ilipokuwa ikipitia Makadirio ya Mapato kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kupitia vyanzo vya makusanyo, Kamati imeshangazwa kwa kuona kifungu **1422078** kinachohusiana na Ukodishaji wa Maeneo ya Kibiashara kimepangiwa kukusanya kwa mwaka mzima wa fedha jumla ya TSh. Milioni 10,000,000/= ambapo ukilinganisha na mwaka 2021/2022 chanzo hiki kilipangiwa kukusanya TSh. Milioni 900,100,000/= wakati hadi tunafikia kupokea taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka huo wa fedha zilizokusanywa TSh. Milioni 4,000,000/= sawa na asilimia 0.4.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Afisi ya Rais, Fedha na Mipango wakati wanapokaa kupanga Mapato ya Serikali ni vyema kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa Wizara husika, kwa sababu wao ndio wanaofahamu uhalisia wa makusanyo kwa vyanzo vinavyokadiriwa kukusanya. Kwani kutokufanya hivyo, inaonekana wazi Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango huwakadiria Mapato yasiyokuwa na uhalisia kwa Wizara za Serikali.

## PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,**
Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Hifadhi ya Jamii ambapo kifungu cha **(SH0401)** katika utekelezaji wa kifungu hiki mwaka 2021/2022 kilitengwa jumla ya TSh. 3,900,000,000/= kwa ajili ya Mradi wa Maendeleo wa Kutoa Huduma za Ustawi wa Jamii, ambapo hadi tunawasilisha taarifa hii ya Bajeti fedha hizo hazikupatikana.

**Mheshimiwa Spika,**
Kamati yangu haikuridhishwa na utaratibu unaotumika na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa kuhaulisha fedha za Miradi zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika Bajeti ya mwaka 2021/2022 kwa baadhi ya Wizara kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha na Miradi hiyo kupangwa tena katika Bajeti hii ya mwaka 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa mnasaba huo, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala hilo kwa umakini mkubwa, kwani inaonekana Serikali inapanga bajeti isiyoweza kutekelezeka kwa mwaka husika, hali inayopelekea miradi mingi kushindwa kutekelezwa kwa wakati uliopangwa. Mfano halisi, Mradi wa Ujenzi wa Uzio kwa Nyumba za Wazee Welezo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

**Mheshimiwa Spika,**
Programu hii inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Uratibu wa Maendeleo ya Jinsia na Watoto **(SH040301),** kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Programu hii ilipangiwa shilingi Milioni 838,038,000/= ukilinganisha na Bajeti ya mwaka 2022/2023 Programu Ndogo hiyo imepangiwa shilingi Bilioni 1,358,154,000/=.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na ongezeko hilo, Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuwaongezea fedha hizo katika huduma **(HH04030101)** Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia.

**Mheshimiwa Spika,**
Licha ya kupangiwa Bajeti kubwa ya kukabiliana na vitendo hivyo, bado takwimu zinazotolewa na Serikali zinahusiana na vitendo hivyo vinaongezeka katika jamii siku hadi siku, ambapo ukiangalia mwaka 2020 jumla ya kesi zilizoripotiwa za ubakaji ni 571 na kwa mwaka 2021 ni 621. Kwa upande wa kesi za ulawiti ni 102 kwa mwaka 2020 na 177 kwa mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,**
Kutokana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kukaa na Taasisi zote husika zinazoshughulikia masuala ya Vitendo vya Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia ikiwemo Jeshi la Polisi, Ofisi ya Muendesha Mashtaka (DPP), Mahkama, Madaktari pamoja na Idara ya Ustawi wa Jamii kwa ajili ya kuupitia upya Mpango Mkakati unaohusiana na Masuala ya Udhalilishaji wa mwaka 2017 hadi 2021, kwa lengo la kuboresha mbinu za kukabiliana na masuala hayo na hatimae kuondosha kabisa vitendo hivyo katika jamii yetu.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI

Mheshimiwa Spika,
Kamati yangu pia imegundua kuwepo kwa changamoto ya uhaba wa watendaji kwa Wizara hii kwa Unguja na Pemba katika ngazi tofauti za utendaji ikiwemo Katibu Mkuu wa Wizara, kutokuwepo kwa Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara, Mhasibu Mkuu wa Wizara na baadhi ya Kurugenzi nyengine muhimu za Wizara hiyo. Hali inayopelekea Wizara hii kufanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika,
Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala hili kwa ukaribu kwa lengo la kupatikana watendaji hao ili Wizara kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo pamoja na Taratibu za Nchi zilizopo.

### Hitimisho

Mwisho kabisa, napenda kukushukuru tena, wewe binafsi, **Mheshimwa Spika**, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni kwa niaba ya Kamati yangu, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini mkubwa, sasa niwaombe Wajumbe wa Baraza lako waijadili na hatimae waiunge mkono bajeti hii, ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka huu wa Fedha unaokuja 2022/2023.

Mheshimiwa Spika,
Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya Kamati ninayoiongoza ya Ustawi wa Jamii, naiunga mkono hoja kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika,

Baada ya Maelezo hayo, **naomba kuwasilisha.**

Ahsante,

……………………………

**Mhe. Mohamed Ahmada Salum,**
**Mwenyekiti,**
**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar.**